Muhtasari jumla

- Utafiti huu ulihamasishwa na ushahidi unaojitokeza, kwamba mashirika yanayoongozwa na wakimbizi (RLOs) katika eneo la Afrika Mashariki huchangia jukumu muhimu katika kukidhi mahitaji ya jamii. Ingawa kumekuwa na ushahidi kuhusu mandhari na shughuli za mashirika ya RLO, hakuna utafiti wa awali ulio wahusisha wanajamii na walengwa wa mashirika haya ili kuelewa jinsi wanavyo tambua athari ya mashirika haya katika jumuiya zao wenyewe. Utafiti huu uliongozwa kuanzia mwanzo hadi mwisho na mtafiti aliye na madharinyuma ya uhamisho.
- Ukusanyaji wa data ulifanyika Nairobi, Kambi ya Wakimbizi ya Kakuma, na makazi jumuishi ya Kalobeyei. Matokeo ya utafiti huu yanatokana na uchunguzi wa kina wa mashirika ya RLOs 15 kupitia mahojiano (KIIs) na viongozi wa mashirika ya RLO, mahojiano na wadau 14 wa nje, majadiliano na vikundi lengwa 30 na wanufaishwa wa mashirika ya RLO na wanajamii, na majadiliano na vikundi lengwa 15 na wasimamizi, wafanyikazi, na watu wa kujitolea katika mashirika ya RLO.
- Mashirika ya RLO nchini Kenya ni ya aina anuwai; yanaanzia kwenye vikundi vidogo na vyama katika jamii mbalimbali hadi kwenye mashirika makubwa zaidi yaliyosajiliwa kama mashirika yanayofanya kazi za kijamii (CBOs) ama mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs). Vikundi vingine pia vinajumuisha mashirika rasmi na yasiyo rasmi ya kidini na vikundi vya kuweka akiba.
- Wakimbizi nchini Kenya huunda mashirika ya RLO ili kujaza mapengo yaliyoachwa na mashirika ya kutoa misaada na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) katika utoaji huduma. Katika maeneo ya mijini, mashirika ya RLO ni mahali pa kwanza ambapo wakimbizi wanaowasili huripoti, na baadhi huwapa wakimbizi wasio na uwezo wa kulipa kodi nyumba salama.
- Mashirika ya RLO hutoa huduma za kielimu (elimu ya watu wazima, mafunzo ya Kiingereza na mafunzo ya dijitali), kazi, usafi wa kibinafsi na wa mazingira, na kilimo, hasa kwenye kambi. Mashirika ya RLO yaliyo mijini na kwenye kambi yalitekeleza jukumu muhimu katika usambazaji wa chakula na vitu vingine muhimu wakati wa mkurupuko wa UVIKO-19. Mashirika mengi rasmi ya RLO yanaongozwa na Wakongo walioelimika. Hii ni kwa sababu wana mitandao pana ilhali jamii zingine hutegemea vyama vya kikabila visivyo rasmi. Hata hivyo, mashirika ya RLO yaongozwayo na Wakongo mara nyingi huajiri raia wa mataifa mengine na wataalamu kutoka jamii mwenyeji kama wafanyikazi. Katika maeneo ambayo wakimbizi huwa wanatoka katika taifa moja, mara nyingi mashirika ya RLO huanzishwa na watu wa taifa hilo.
- Mashirika mengi ya RLO huundwa na wanaume na kuna vikundi vichache vinavyongozwa na wanawake. Hii ni kutokana na vikwazo vya kimuundo na kitamaduni ambavyo wanawake wengi hukabiliana navyo. Wanawake wana miunganisho ya mtandao chache , mara nyingi hawajumuishwi katika kufanya maamuzi na wengi wana elimu isiyo rasmi pekee.
- Katika maeneo ya mijini, mashirika ya RLO yanajulikana na jamii za wakimbizi ndani ya eneo lao la kazi. Katika maeneo ambayo kuna wakimbizi wachache, kwa kawaida hawajui kuhusu kuwepo kwa mashirika ya RLO. Katika mazingira ya kambi, mashirika ya RLO yanajulikana sana, hasa mashirika ya RLO aali na makubwa. Vijana hufahamu mashirika

mengi ya RLO.

- Maafisa wa serikali walio katika kambi, kama vile Idara ya Huduma kwa Wakimbizi (DRS), wanafahamu mashirika ya RLO yaliyosajiliwa na ambayo hayajasajiliwa kwani wanasimamia usajili wa mashirika ya kutoa huduma katika jamii (CBO). Katika maeneo ya mijini, machifu wa hapo na polisi hufahamumashirika ya RLO. Chifu husimamia usajili, na wakati mwingine polisi hushauriana na baadhi ya mashirika ya RLO ikiwa mkimbizi anashutumiwa kwa kutenda kosa.
- Mashirika yasiyo ya serikali na shirika la UNHCR yanafahamu kuwepo kwa mashirika makubwa zaidi ya RLO katika maeneo ya mijini na kambini.
- Michango ya wanachama huwezesha uanzishaji wa baadhi ya mashirika mengi ya RLO. Shughuli zinazofuata huleta riba na ufadhili kutoka kwa mashirika yasiyo ya serikali na wafadhili kutoka nje, na michango ya wanachama inaweza kusimamishwa. Baadhi ya mashirika ya RLO hupata fedha kutoka kwa ufadhili wa mtandaoni, misaada kutoka nje ya nchi na michango kutokana na shughuli kama vile miradi ya kupata riziki ama shughuli za kitamaduni.
- Mashirika ya RLO ambayo yanajulikana sana na yana mitandao mipana hujulikana kama mashirika ya RLO ya ngazi ya aali. Katika kambi na maeneo ya mijini,mashirika haya ya RLO aali ni sehemu ya mashirika kama RELON-Kenya.
- Wanufaishwa hueleza utoaji wa huduma wa mashirika ya RLO kuwa wa haraka na bora. Wengine wanasema kwamba wanatendewa kwa uelewa na heshima, na wengine huongeza kusema kuwa huduma za mashirika ya RLO hukidhi mahitaji yao. Hata hivyo, wanawake na wazee wanahisi kuwa wametengwa katika huduma kwani mengi hulenga vijana. Watu wengine wasionufaika katika jamii wanahisi kuwa mashirika ya RLO yaliyoanzishwa na kabila fulani yanaweza kuwalenga tu wale wa kabila moja.
- Jamii ya wakimbizi inazingatia utoaji wa huduma kwa mashirika ya RLO kama unaopatikana kwa urahisi zaidi kwa sababu, kinyume na mashirika ya misaada na UNHCR, mashirika ya RLO huundwa katiya jamii. Mashirika ya RLO huruhusu wanufaika kutumia lugha yao asili na kuwapa usaidizi licha ya changamoto za kuweka rekodi, tofauti na mashirika yasiyo ya serikali na UNHCR. Baadhi wanahisi kuwa mashirika ya RLO hulenga zaidi wanufaishwa na kuunda kazi zinazolipa zaidi kwa wakimbizi kuliko NGOs na UNHCR.
- Viongozi na wanufaika wa mashirika ya RLO na baadhi ya washikadau kutoka nje wanachukulia mashirika ya RLO kuwa na athari kubwa kwa sababu ya ukaribu na uwezo wao wa kuielewa vyema jamii. Mashirika ya RLO ni mahali pa kwanza ambapo wanaowasili huripoti katika maeneo ya mijini na ni vituo muhimu vya kuenezahabari kuhusu wakimbizi. Jambo hili lilionekana hasa wakati wa UVIKO-19 wakati mashirika ya RLO yalichukua kipao mbele katika utoaji wa huduma.
- Athari za mashirika ya RLO nchini Kenya hutegemea ufikiaji wa mitandao na mfumo wa udhibiti. Viongozi wa mashirika ya RLO wenye uhusiano wa awali na shirika la UNHCR na mashirika mengine ya misaada wanaweza kupata fedha kutoka kwa mashirika yasiyo ya serikali, shirika la UNHCR na nchi za nje; na viongozi wa mashirika ya RLO wenye uhusiano na maafisa wa serikali wanaweza wakapata usajili. Mashirika ya RLO ambayo yamesajiliwa yanaweza kutuma maombi ya ufadhili kutoka nje na wakati mwingine hufanya kazi kwa ushirikiano na mashirika yasiyo ya serikali, wakati mashirika ya RLO ambayo hayajasajiliwa

yanakabiliwa na changamoto wanapotuma maombi ya ufadhili na ruzuku.

- Mashirika ya RLO nchini Kenya yana upungufu wa ushirikiano wa maana na mashirika yasiyo ya serikali auUNHCR; hata hivyo, baadhi ya mashirika ya RLO hupokea ruzuku kutoka kwa mashirika yasiyo ya serikali ili kutekeleza miradi.
- Changamoto ambazo mashirika ya RLO hukabiliana nazo ni pamoja na upungufu wa kifedha, ukosefu wa usajili, ukosefu wa uwezo wa kuwaongeza ujuzi wafanyakazi na viongozi wa mashirika ya RLO, na urudufishaji wa huduma kutoka kwa mashirika mengi ya RLO.
- Hatua ambazo mashirika ya RLO yamechukua ili kukabiliana na changamoto ni pamoja na kuingiliana zaidi kati ya mashirika ya RLO na mitandao ya RLO ili kupata ufahamu na kushirikiana katika miradi. Baadhi ya mashirika ya RLOs hufanya shughuli za kuzalisha mapato kama vile kutumbuiza watu kwenye harusi na kusambaza umeme katika kambi.

Mapendekezo

- Wafadhili wanafaa kutoa ufadhili ulio wa hali ya juu, ufadhili nyoofu na wa muda mrefu kwa mashirika ya RLO. Zaidi ya hayo, wanafaa kuzingatia kufadhili vikundi vya kibinafsi vinavyoongozwa na wakimbizi ili kuwasaidia kukua.
- Serikali yapaswa kurahisisha na kuwasiliana mwendo wa usajili. Serikali zinafaa kufanya usajili taratibu, moja kwa moja na kuwasiliana mapema hatua zinazo takikana kusajili. UNHCR yapaswa kuboresha njia za mawasiliano na mashirika ya RLO na kusambaza maarifa kuhusu fursa kwa mashirika haya kwa njia zinazo zingatia mahitaji yao.
- Mashirika ya usaidizi yafaa kuwahusisha mashirika ya RLO katika kufanya maamuzi kupitia miungano yeneye ushirika sawa, na kukuza uendelezaji wa uwezo kutumia miradi iliyofadhiliwa ndiposa waweze kuona matokeo yanayo pana muda mrefu. Mashirika ya usaidizi yanafaa pia kuweka timu za washauri wanaoptakina kwa urahisi, washauri wanaoweza kusaidia mashirika ya RLO kueleza na kukuza miradi yao na kuhakikisha kuwa yanaambatana na matako ya wafadhili.
- Mashirika ya RLO yaliyo na ufikiaja bora kwa mitandao wanapawa kuwahusisha mashirika ya RLO madogo, ambayo hayajaendelea sana katika utoaji wa huduma. Wanapaswa kukuza ushirikiano sawa nao ilimradi kuwezesha ufikiaji na washirika na rasilimali. Mashirika ya RLO yanafaa pia kukuza mifumo ya ukuzaji and usambasaji wa kumbukumbu katika kiwango ya kijamii.
- Mashirika ya RLO yanapaswa kufanya juhudi zilizo wazi ili kuwahusisha makundi mbalimbali yaliyotengwa katika miundo yao.
- Usaidizi unaohitajika na mashirika ya RLO ni pamoja na kuongezeka kwa ufadhili na kuzingatia fursa za ufadhili za muda mrefu. Mashirika ya RLO pia yanahitaji mafunzo ya uwezeshaji na ujuzi kwa wafanyakazi, ushirikiano na mashirika mengine yasiyo ya serikali na UNHCR na usaidizi wa nyaraka na usajili.